

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram "AFYA", DODOMA  
Nambari ya Simu: +255 026 – 2323267  
E- Mail Na. [ps@afya.go.tz](mailto:ps@afya.go.tz)



Mji wa Serikali Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S.L. P 743,  
40478 DODOMA.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**TAARIFA YA MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI**

**Dar es Salaam, Ijumaa Aprili 03, 2020**

***“MGONJWA WA TATU WA CORONA ALIYEKUWA ANAPATA MATIBABU NGARA AMEPONA, MKOA WA KAGERA HAUNA MGONJWA,***

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatoa taarifa kuwa mgonjwa mmoja aliyekuwa katika kituo cha matibabu Wilaya ya Ngara mkoani Kagera amethibitika kupona ugonjwa wa Corona (COVID-19) na kufanya mkoa huo kutokuwa na mgonjwa kwa sasa .

Kupona kwa mgonjwa huyo wa tatu (3), mwanaume, mwenye historia ya kutembelea kikazi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Congo (DRC) na Burundi kabla ya kukutwa na maambukizi aliporejea nchini, kunaifanya Tanzania kubaki na wagonjwa **Kumi na Sita (16)** wa Corona (COVID 19) waliopo Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar wakiendelea na matibabu na hali zao ni nzuri.

Taarifa za vipimo kutoka Maabara Kuu ya Taifa nchini pia zinaonyesha mgonjwa pekee wa Arusha kwa sasa kutokuwa na maambukizi ikiwa ni siku Tisa baada ya kuanza matibabu ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID 19). Mgonjwa huyo anaendelea kuwa chini ya uangalizi hadi atakapochukuliwa vipimo vingine siku ya 14 ya matibabu yake kuthibitisha kuwa hana tena virusi vya corona ndipo atakapotangazwa kuwa amepona.

Aidha, Serikali inawahakikishia watumishi wa sekta ya Afya kuwa kipaumbele chake cha kwanza katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona (COVID-19) ni kuwalinda watumishi wa afya ambao wako mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo kwa kuwapatia vifaa kinga ili wasipate maambukizi wakati wanatoa huduma kwa wagonjwa.

Hivi karibuni, Serikali ilipokea vifaa tiba vikiwemo barakoa (mask), gloves na mavazi ya kujikinga na maambukizi (Personal Protective Equipment-PPE) kutoka kwa mfanyabiashara maarufu wa China, Jack Ma. Asilimia 90 ya vifaa hivyo vitapelekwa kwa watoa huduma za Afya nchini na vifaa vingine vitatolewa kwa maeneo yanayotoa huduma kwa jamii wakiwemo Magereza na Polisi.

Hivyo, kwa kuanzia, Wizara leo imetoa jumla ya Barakoa 16,000, Gloves 8,000, Mavazi ya kujikinga na maambukizi pamoja na Vidonge vya Chlorine kwa ajili ya kutengeneza vitakasa mikono kwa Jeshi la Polisi na Magereza ambao wamekuwa wakikutana na wananchi wakati wakitekeleza majukumu yao ya kila siku.

Pamoja na kutoa vifaa kinga, Serikali itatoa mafunzo kwa watumishi wa majeshi ya Magereza na Polisi ya namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona (COVID - 19) wakati wakitekeleza majukumu yao yanayowakutanisha na wananchi kila siku.

Serikali inawapongeza wananchi kwa kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona (COVID- 19) hususan kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka. Hata hivyo, tunawasisitiza wananchi pia kuzingatia maelekezo mengine yanayohusu kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima na kukaa umbali usiopungua mita moja kati ya mtu na mtu.



Ummy A. Mwalimu (Mb)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**